



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**MWALIKO WA WATAZAMAJI WA UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI
KATIKA KATA 43 KWENYE HALMASHAURI MBALIMBALI TANZANIA BARA**

Kwa mujibu wa kifungu cha 13 (3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi Mdogo wa Madiwani katika Kata 43 kwenye Halmashauri mbalimbali Tanzania Bara, kujaza nafasi wazi kwenye Kata hizo zilizo wazi kutokana na sababu mbalimbali.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia Kanuni ya 14 (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 2015, inapenda kualika Asasi za Kiraia na Taasisi mbalimbali za ndani zinazotaka kuwa Watazamaji wa Uchaguzi katika Uchaguzi Mdogo unaotarajiwa kufanyika tarehe **26 Novemba, 2017**.

Ratiba ya Uchaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Tukio | Tarehe |
|-----|----------------------------|---------------------------------------|
| 1. | Kutoa Fomu za Uteuzi | 20 Oktoba, 2017 hadi 26 Oktoba, 2017 |
| 2. | Siku ya Uteuzi wa Wagombea | 26 Oktoba, 2017 |
| 3. | Kampani za Uchaguzi | 27 Oktoba, 2017 hadi 25 Novemba, 2017 |
| 4. | Siku ya Kupiga Kura | 26 Novemba, 2017 |

Kata zitakazofanya Uchaguzi ni kama ifuatavyo:-

| NA. | KATA | HALMASHAURI/JIJI/MANISPAA/MJI/WILAYA |
|-----|-------------------|--------------------------------------|
| 1 | Muriet | Halmashauri ya Jiji la Arusha |
| 2 | Musa | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha |
| 3 | Mamba | Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli |
| 4 | Senga | Halmashauri ya Wilaya ya Geita |
| 5 | Machame Magharibi | Halmashauri ya Wilaya ya Hai |
| 6 | Mnadani | Halmashauri ya Wilaya ya Hai |
| 7 | Weruweru | Halmashauri ya Wilaya ya Hai |
| 8 | Nangwa | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang |
| 9 | Siuyu | Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi |
| 10 | Kitwiru | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa |
| 11 | Kimala | Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo |
| 12 | Mbweni | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| 13 | Majengo | Halmashauri ya Mji wa Korogwe |
| 14 | Chikonji | Halmashauri ya Manispaa ya Lindi |
| 15 | Lunguza | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto |
| 16 | Sofi | Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi |
| 17 | Chanikanguo | Halmashauri ya Mji wa Masasi |
| 18 | Nyabubinza | Halmashauri ya Wilaya ya Maswa |
| 19 | Muongozi | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga |
| 20 | Ambureni | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
| 21 | Leguruki | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
| 22 | Makiba | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
| 23 | Maroroni | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
| 24 | Ngabogo | Halmashauri ya Wilaya ya Meru |
| 25 | Kijima | Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi |
| 26 | Ndalambo | Halmashauri ya Wilaya ya Momba |
| 27 | Moita | Halmashauri ya Wilaya ya Monduli |
| 28 | Kiloka | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro |

| NA. | KATA | HALMASHAURI/JIJI/MANISPAA/MJI/WILAYA |
|-----|------------|------------------------------------------------|
| 29 | Bomambuzi | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi |
| 30 | Chipogolo | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa |
| 31 | Reli | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani |
| 32 | Mhandu | Halmashauri ya Jiji la Mwanza |
| 33 | Bukwimba | Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'wale |
| 34 | Nata | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega |
| 35 | Mnacho | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa |
| 36 | Ibighi | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe |
| 37 | Sumbawanga | Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga |
| 38 | Milongodi | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba |
| 39 | Kijichi | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| 40 | Kalulu | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |
| 41 | Lukumbule | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |
| 42 | Saranga | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| 43 | Muungano | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo |

Asasi/Taasisi zinapaswa kuzingatia masharti yafuatayo wakati wa kuwasilisha maombi yao:-

- (i) Anuani Kamili ya Asasi inayotaka kutazama Uchaguzi,
- (ii) Mahali Asasi husika inapofanyia shughuli zake,
- (iii) Shughuli zinazofanywa na Asasi husika,
- (iv) Kata ambayo Asasi hiyo inataka kutazama Uchaguzi,
- (v) Idadi ya Watu itakaowatumia kutazama Uchaguzi, na
- (vi) Majina ya Viongozi wa Asasi husika kama yalivyoandikwa katika Nyaraka za Usajili wa Asasi/Taasisi hiyo.

Aidha, Asasi husika itatakiwa kuambatanisha nakala za nyaraka za uandikishaji/usajili wa Asasi hiyo.

Maombi ya kuwa Watazamaji wa Uchaguzi yataapaswa kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Makao Makuu kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Posta House, Ghorofa ya 7,
Mtaa wa Ghana/Ohio,
S. L. P. 10923,

DAR ES SALAAM.

Mara baada ya Tume kupokea Maombi ya Taasisi/Asasi husika, itayapitia na kisha kuitaarifu iwapo imekubaliwa au imekataliwa. Maombi yatatakiwa kuwasilishwa si zaidi ya tarehe 16 Novemba, 2017.

Limetolewa na:-

Kailima R. K

MKURUGENZI WA UCHAGUZI